Australian Government

# Uraia wa Australia

## Mapatano yetu ya Pamoja







*Kuanzia wakati huu na kuendelea,*

*Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,*

*ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,*

*ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na*

*ambao nitafuata na kutii sheria zao.*

# Uraia wa Australia

## Mapatano yetu ya Pamoja

Maelezo yote unayoyahitaji ili kufanya mtihani wa uraia wa Australia yako katika kitabu hiki. Hauhitajiki kununua au kupata vifurushi vingine vya uraia kutoka kwa mtu au shirika lolote ili kupita mtihani wa uraia. Idara haiidhinishi au kupendekeza kifurushi chochote ambacho kinadaiwa kukusaidia kupita mtihani wa uraia.

© Commonwealth of Australia 2009

Kazi hii ina hakimiliki. Unaweza kupakua, kuangazisha, kuchapisha na kutoa tena nyenzo hii katika hali isiyobadilika pekee (ukibaki na notisi hii) kwa utumizi wako binafsi, usio wa kibiashara au utumizi katika shirika lako. Mbali na utumizi wowote kama ilivyoruhusiwa chini ya *Sheria ya Hakimiliki ya 1968 (Copyright Act 1968),* haki zote zingine zimehifadhiwa.

Maombi ya uidhinishaji zaidi yanapaswa kuelekezwa kwa:
Commonwealth Copyright Administration
Copyright Law Branch
Attorney-General's Department
Robert Garran Offices
National Circuit
Barton ACT 2600

Faksi: 02 6250 5989
Barua pepe: commonwealth.copyright@ag.gov.au

Imechapishwa na Tawi la Mawasiliano la Kitaifa la Idara ya Uhamiaji na Uraia (National Communications Branch of the Department of Immigration and Citizenship)

6 Chan Street Belconnen ACT 2617

ISBN 978-1-92446-96-2

Kanusho:
Wasomaji wa asili na wa visiwa vya Torres Strait wanaonywa kwamba toleo hili lina picha na/au yaliyomo yanayohusiana na watu waliokufa.

# Yaliyomo

Ujumbe wako 3

## Sehemu inayoweza kujaribiwa

Sehemu ya 1 – Australia na watu wake 8

Sehemu ya 2 – Imani ya demokrasia, haki na uhuru wa Australia 16

Sehemu ya 3 – Serikali na sheria huko Australia 22

Faharasa ya sehemu inayoweza kujaribiwa 30

Maswali ya mazoezi ya jaribio 34

## Sehemu isiyoweza kujaribiwa

Sehemu ya 4 – Australia leo 38

Sehemu ya 5 – Hadithi yetu ya Australia 54

Faharasa ya sehemu isiyoweza kujaribiwa 72

Kwa maelezo zaidi 74

Shukrani 76




*Uraia wa Australia ni fursa inayotoa thawabu anuwai.*
*Kwa kuwa raia wa Australia, unaungana na jamii ya kipekee ya kitaifa.*

# Ujumbe kwako

Hongera kwa kuchagua kuwa raia wa Australia. Inahitaji ujasiri, kuvumilia na kujitolea kuishi katika nchi geni na kuhusika kikamilifu kama raia. Tunathamini mchango wako kwa jamii yetu yenye amani na demokrasia.

Uraia wa Australia ni hatua muhimu katika hadithi yako ya uhamiaji. Kuwa raia wa Australia inamaanisha kwamba unaendelea kujitolea kwa Australia na yote ambayo nchi hii inamaanisha. Pia ni mwanzo wa uanachama wako rasmi wa jamii ya Australia. Ni hatua ambayo itakuwezesha kusema 'Mimi ni Mwaustralia'.

Uraia wa Australia ni fursa inayotoa thawabu anuwai. Kwa kuwa raia wa Australia, unaungana na jamii ya kipekee ya kitaifa. Nchi yetu imejengwa kwenye michango michanganyiko ya watu wetu wa asili na wale ambao walikuja baadaye kutoka ulimwengu wote. Tunasherehekea utofauti na kwa wakati huo huo, tunang'angan'ia taifa lenye umoja na usawa.

Nguvu ya jamii ya Australia inamaanisha kwamba tunafanya kazi pamoja kutatua matatizo na kufanya Australia nchi nzuri ilivyo. Tuna mfumo thabiti wa serikali na Waaustralia wanaheshimu mamlaka na sheria za serikali. Uthabiti wetu, utamaduni wetu na sheria zetu zimeundwa na historia yetu. Kwa kujiunga na jamii ya Australia, utarithi historia hii na utakuwa kwenye nafasi ya kuichangia.

Australia ni nchi ya zamani. Ni kubwa na ya kipekee. Ni nchi ya misitu ya mvua na misitu; ya ufuo za rangi ya dhahabu na jangwa zilizokauka. Tamaduni zetu za asili ndizo za zamani kabisa zinazoendelea katika ulimwengu. Sisi pia ni taifa changa; taifa la wahamiaji. Makazi ya waulaya hapa Australia yalianza mnamo 1788 na tunaendelea kukaribisha wahamiaji wapya leo. Watu kutoka kwa zaidi ya nchi 200 wamefanya Australia kuwa nyumbani kwao. Hivyo basi, jamii yetu ni moja ya zile zilizo anuwai zaidi ulimwenguni. Australia inajumuisha asili ya kikabila na kitamaduni anuwai na umoja wa kitaifa. Uraia ni umoja unaotuunganisha sisi sote.

Australia ni demokrasia. Uraia hukupa fursa ya kuhusika kikamilifu katika kujenga taifa letu la kidemokrasia. Inamaanisha kwamba uko tayari kutimiza wajibu wako kama mwanachama rasmi wa jamii ya Australia. Watu wa Australia wanaamini uadilifu na uhuru wa kila mtu, ubora wa wanaume na wanawake na utawala wa sheria. Uraia wa Australia ni juu ya kuishi kutoka kwa thamani hizi katika maisha yako ya kilasiku.

## Kiapo cha Uraia wa Australia

Ni muhimu kwa raia wote wa Australia kuelewa haki zetu na wajibu wetu na inamaanisha nini kuwa raia, ikiwa sisi ni wa Australia kwa kuzaliwa au kwa kuchagua. Ni sehemu muhimu ya kujenga taifa letu.

Wakati unahudhuria hafla ya uraia wa Australia, utachukua Kiapo cha Uraia wa Australia. Kwa kufanya hivyo, unajitolea kwa umma kwa Australia na kukubali wajibu na fursa za uraia. Kujifunza juu ya maana ya Kiapo kutakupa kuelewa zaidi inamaanisha nini kuwa raia wa Australia na wajibu na fusra za uraia.

Hiki ndicho kiapo utakachochukua:

*Kuanzia wakati huu na kuendelea, chini ya Mwenyezi Mungu,**

*Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,*

*ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,*

*ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na*

*ambao nitafuata na kutii sheria zao.*

* Mtu anaweza kuchagua ikiwa atatumia maneno 'chini ya Mwenyezi Mungu'.

Unaposoma kitabu hiki, utapata kuelewa kikamilifu maana ya Kiapo na jinsi unaweza kuboresha wajibu wako katika jamii ya Australia.

# Kuwa raia wa Australia

Historia ya uhamiaji ya Australia ina zaidi ya miaka 200. Kwa njia hii, sisi bado ni taifa changa na wewe ni sehemu ya hadithi yetu. Maamuzi unayofanya kama raia wa Australia yatakusaidia kuunda siku zetu za usoni.

## Jaribio la uraia wa Australia

Jaribio la uraia wa Australia limeundwa kuchunguza ikiwa una ufahamu wa kutosha juu ya Australia na wajibu na fursa za uraia.

Jaribio la uraia pia limeundwa kuchunguza ikiwa una maarifa ya msingi ya lugha ya Kiingereza. Kiingereza ni lugha yetu ya taifa. Kuwasiliana kwa Kiingereza hukusaidia kuwa na jukumu amilifu zaidi katika jamii ya Australia. Hukusaidia kutumia elimu, ajira na fursa zingine kikamilifu ambazo Australia inatoa.

Jaribio la uraia ni jaribio la kompyuta lenye majibu mengi kwa Kiingereza. Jaribio la uraia lina maswali 20 yaliyotolewa kutoka kwa maswali mengi bila taratibu. Ili kupita jaribio, lazima ujibu asilimia 75, au 15 ya maswali 20, kwa usahihi.

Majaribio ya uraia hufanywa katika ofisi za Idara ya Uhamiaji na Uraia kote Australia. Majaribio pia yamepangwa katika maeneo kadhaa kote katika mikoa wa Australia na katika baadhi ya balozi za nchi za ng'ambo.

Kwa kupita jaribio la uraia, utakuwa umeonyesha kwamba unaelewa kujitolea ambao unafanya kwa kuchukua Kiapo cha Uraia wa Australia.

## Kujiandaa kwa jaribio la uraia wa Australia

Kujiandaa kwa jaribio la uraia utahitaji kusoma kitabu hiki cha msaada.

### Kitabu cha msaada

Kitabu hiki cha msaada kina sehemu inayoweza kujaribiwa na isiyoweza kujaribiwa.

### Sehemu inayoweza kujaribiwa

Maelezo yote unayohitaji kujua kupita majaribio ya uraia yako katika sehemu tatu za kwanza za kitabu hiki:

- Semehu ya 1 – Australia na watu wake
- Sehemu ya 2 – Imani ya demokrasia, haki na uhuru wa Australia
- Sehemu ya 3 – Serikali na sheria huko Australia

Utahitajika kujua na kuelewa maelezo katika sehemu inayoweza kujaribiwa ili kujibu maswali katika jaribio la uraia.

### Sehemu isiyoweza kujaribiwa

Sehemu isiyoweza kujaribiwa ina maelezo muhimu ambayo yatakusaidia kuelewa historia na utamaduni wa Australia. Hautajaribiwa juu ya maelezo haya.

- Sehemu ya 4 – Australia leo
- Sehemu ya 5 – Historia yetu ya Australia

### Maswali ya mazoezi

Mwisho wa sehemu inayoweza kujaribiwa, kuna maswali 20 ya mazoezi ili kukusaidia kujiandaa kwa jaribio la uraia.

### Faharasa

Kuna faharasa (orodha ya maneno kuu na maana yao) mwisho wa sehemu zinazoweza kujaribiwa na zisizoweza kujaribiwa.

### Matoleo yaliyotafsiriwa ya kitabu hiki cha rasilimali

Kitabu hiki cha msaada kimetafsiriwa katika lugha 37 za jamii kwa hao raia wanaotarajiwa ambao wana ustadi zaidi wa kusoma katika lugha nyingine mbali na Kiingereza. Tafsiri hizi zinapatikana kwa upakuzi kutoka kwa tovuti ya uraia wa Australia pekee www.citizenship.gov.au.

## DVD

DVD sikizi-onyeshi katika Kiingereza pia inapatikana kusaidia raia wanaotarajiwa kujiandaa kwa jaribio la uraia. Kwenye DVD utapata wasilisho la vidokezo muhimu kutoka kwa sehemu inayoweza kujaribiwa, na pia maswali 20 ya mazoezi ya jaribio. DVD hii imetolewa kama kifaa cha kujifunza kwa wale wateja wenye ustadi mdogo wa lugha ya Kiingereza. DVD inapatikana kwa agizo au kwa kupakua kutoka kwa tovuti ya uraia wa Australia www.citizenship.gov.org.au.

## Msaada wakati wa jaribio la uraia wa Australia

Inatarajiwa kwamba raia wengi wanaotarajiwa wa Australia watakuwa na ustadi wa kusoma na kuandika unaofaa kukamilisha jaribio la uraia bila msaada. Kwa wale watu ambao wanahitaji msaada kwa sababu ya ustadi mdogo wa kuandika na kusoma Kiingereza, afisa anaweza kusaidia kwa kusoma maswali na majibu yanayowezekana kwa sauti. Msaada pia utapatikana kwa watu ambao wana viwango ndogo vya ustadi wa kompyuta, au ambao wana ulemavu. Ikiwa unafikiri utahitaji msaada wakati wa jaribio la uraia, tafadhali shauri afisa wa uraia.

## Mapatano yetu ya Pamoja: Kozi ya Uraia wa Australia

Unaweza kustahiki kuhudhuria kozi ya uraia wa Australia badala ya jaribio la kutumia kompyuta.

Kozi ya uraia itapitia maelezo yote katika sehemu ya kitabu hiki inayoweza kujaribiwa. Bado unahitaji kuonyesha kwamba una maarifa ya msingi ya Kiingereza na unaelewa mawazo katika Kiapo cha Uraia wa Australia.

Kwa maelezo kuhusu kozi inapatikana kutoka kwa tovuti ya uraia wa Australia www.citizenship.gov.au.

## Kwa maelezo zaidi

Unaweza kupiga simu kwa laini ya maelezo ya Uraia katika 131 880 (Jumatatu hadi Ijumaa 8.30am to 4.30 pm, yaani saa mbili na nusu asubuhi hadi saa kumi na nusu jioni).

Ikiwa unahitaji huduma ya mkalimani, tafadhali piga simu kwa 131 450.

Unaweza pia kutembelea tovuti ya uraia wa Australia www.citizenship.gov.au.

## Hafla ya uraia wa Australia

Hafla za Uraia wa Australia zinaweza kuwa ndogo, zikihusisha tu watu wachache, au zinaweza kuwa kubwa sana, zikihusisha mamia au hata maelfu ya watu. Undani wa kuhisi na kujivunia kati ya raia wageni na maafisa huifanya iwe karamu yenye raha sana.

Katika mwanzo wa hafla ya uraia, unaweza kukaribishwa na mwakilishi wa watu wa asili ambao ni wamiliki wa kitamaduni wa ardhi katika eneo lako. Utasikia maneno ya kukaribisha na kuhimiza kutoka kwa viongozi wengine wa jamii ya eneo lako au wawakilishi wa serikali.

Utasoma au kurudia Kiapo cha Uraia wa Australia kwa sauti na watu wengine ambao wamechagua kuwa raia wa Australia. Hivi ni sehemu muhimu sana ya hafla. Hutakuwa raia wa Australia mpaka umeapa kiapo chako cha kuijitolea kwa Australia.Unakaribishwa kuleta kitabu au somo takatifu ili kushika wakatiunapoapa, lakini sio lazima ufanye hivyo.

Viongozi kutoka kwa jamii yako au wawakilishi wa serikali watatoa hotuba fupi juu ya maana ya uraia. Utapokea Cheti cha Uraia wa Australia na unaweza pia kupokea zawadi ndogo kutoka kwa jamii. Kila mtu ataimba wimbo wa taifa wa Australia ‘Endeleza Australia bila mapendeleo (Advance Australia Fair)’. Baada ya hafla ya uraia, utakuwa na fursa ya kukutana na kusherehekea na wenzako wa Australia.

Tunakutakia kila la heri katika kuwa raia wa Australia na katika kutafuta maisha yenye amani na yenye mazao hapa Australia.



Raia wapya wa Australia katika hafla yao ya uraia



# Mwanzo wa sehemu inayoweza kujaribiwa





# Sehemu ya 1
# Australia na watu wake

*Kuanzia wakati huu na kuendelea, chini ya Mwenyezi Mungu,**

***Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,***

*ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,*

*ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na*

*ambao nitafuata na kutii sheria zao.*

** Mtu anaweza kuchagua ikiwa atatumia maneno 'chini ya Mwenyezi Mungu'.*

# Australia na watu wake

Katika hafla ya uraia, unaapa uaminifu wako kwa Australia na watu wake. Kwa hivyo ni muhimu kwako kuwa na kuelewa kwa jamii na idadi ya watu wa Australia, pamoja na urithi wetu wa asili. Ni muhimu pia kwako kuelewa jinsi Australia ilikuwa kutoka kwa mwanzo usio na uhakika kama wakoloni wa Briteni kuwa taifa lenye tamaduni anuwai, thabiti na lenye ufanisi leo.

Katika sehemu hii, utasoma juu ya baadhi ya matukio ambayo yamechangia hadithi yetu. Kuna maelezo kuhusu majimbo yetu na wilaya yetu, na kuna maelezo kuhusu tamaduni na ishara ambazo tunatambua kwa kujivunia kama kuwa ya Australia kipekee.

## Watu wetu

### Watu wa asili ya Australia

Wakazi wa kwanza wa Australia walikuwa watu wa asili na wakazi wa visiwa vya Torres Strait. Wao ndio watu wa asili wa Australia. Tamaduni zetu za asili ndizo za zamani kabisa zinazoendelea katika ulimwengu.

Kihistoria, watu wa asili wanatoka nchi kuu ya Australia na Tasmania. Wameishi hapa kati ya miaka 40 000 na 60 000.

Torres Strait Islanders wanatoka sehemu ya kaskazini mwa Queensland. Wana utambulisho wa kipekee cha kitamaduni.

Watu wa asili wanashiriki imani na tamaduni sawa ambazo bado huwaongoza leo. Wana uhusiano wa ndani na ardhi ambayo huoneshwa katika hadithi, sanaa na kucheza kwao.

### Siku za mapema za makazi ya Waulaya

Makazi ya Ulaya yaliaanza wakati meli za kwanza za wafungwa, ambazo zilikuja kujulikana kama "Kundi la kwanza la Meli(First Fleet), kuwasili kutoka Briteni mnamo 26 Januari 1788.

Wakati huu sheria za Briteni zilikuwa kali na jela hazingeweza kuweka idadi kubwa ya watu waliofungwa kwa uhalifu wao. Kuweza tatizo hili, Serikali ya Briteni iliamua kusafirisha wafungwa hadi upande mwingine wa ulimwengu; kwa koloni mpya ya New South Wales.

Gavana wa kwanza wa koloni ya New South Wales alikuwa Captain Arthur Phillip. Alishinda matatizo mengi katika miaka michache ya kwanza ya makazi ya Ulaya. Koloni ilistahimili na vile wafungwa zaidi na wakazi huru walipofika, ilikuwa kubwa na kuendelea. Koloni zaidi zilianzishwa katika sehemu zingine za nchi.

Wakazi huru wa mapema kutoka Briteni Kuu na Ireland. Urithi wa Briteni na Irishi umekuwa na ushawishi mkubwa kwa historia ya Australia, tamaduni na taasisi za kisiasa.

Mnamo 1851, dhahabu iligunduliwa katika koloni za New South Wales na Viktoria. Watu kutoka ulimwenguni kote walikuja kwa koloni hizi kujaribu bahati yao kwa kutengeneza mali. Watu wa Uchina waliofika wakati huo walikuwa kundi la kwanza la wahamiaji ambao hawakutoka Ulaya. Kwa miaka 10, idadi ilikuwa zaidi ya mara mbili.

### Taifa la Australia

Kwa miongo iliyofuata, koloni tofauti zilijadili wazo la kuwa taifa moja.

Mnamo 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho la majimbo liitwalo Jumuiya ya Madola ya Australia. Wakati huo, idadi ya watu wa Australia ilihesabiwa kuwa karibu watu milioni nne. Idadi hii haikujumuisha watu wa asili.

Wakati wote wa nusu ya kwanza ya karne, viwango vya uhamaji vilipanda na kushuka. Kulikuwa na mipango ya kuhimiza wahamiaji wa Briteni ili kukaa hapa, na wengi walifanya hivyo.

Wimbi la uhamiaji usio wa Briteni ulikuja baada ya Vita vya II vya Dunia, wakati mamilioni ya watu huko Ulaya walilazimika kuacha nchi zao. Idadi kubwa zilikuja Australia kujenga maisha mapya.

Katika miaka ya hivi karibuni, mipango yetu ya uhamaji na ukimbizi imeleta watu Australia kutoka ulimwenguni kote. Watu wamekuja hapa kuungana na familia, kuanza maisha mapya katika nchi changa, au kutoroka umaskini, vita au kuadhibiwa.

Leo, Australia ina idadi ya karibu watu milioni 22. Zaidi ya robo ya watu hawa walizaliwa ngambo. Australia imejazwa na mchango ambao watu hawa wanafanya kwa taifa letu. Wakati tunasherehekea anuwai ya watu wa Australia, tunalenga pia kujenga taifa la kushikana pamoja na yenye umoja.

Kiingereza ni lugha ya taifa la Australia. Ni sehemu ya utambulisho wa kitaifa. Kila mtu hapa Australia anahimizwa kujifunza na kutumia Kiingereza kuwasaidia kuhusika katika jamii ya Australia. Kuwasiliana kwa Kiingereza pia ni muhimu kwa kutafuta mapato na kufanya kazi Australia. Lugha zingine pia zinathaminiwa. Katika jamii anuwai ya Australia, zaidi ya lugha 200 zinazungumzwa.

# Majimbo na wilaya za Australia

Jumuiya ya madola ya Australia ni shirikisho la majimbo na wilaya. Kuna majimbo sita na wilaya mbili za nchi kuu. Canberra ndio mji mkuu wa Australia, na kila jimbo na wilaya ya nchi kuu ina mji mkuu wake.




| Jimbo | Mji mkuu |
|---|---|
| New South Wales (NSW) | Sydney |
| Victoria (Vic.) | Melbourne |
| Queensland (Qld) | Brisbane |
| Western Australia (WA) | Perth |
| South Australia (SA) | Adelaide |
| Tasmania (Tas.) | Hobart |
| **Wilaya** | **Mji mkuu** |
| Australian Capital Territory (ACT) | Canberra |
| Northern Territory (NT) | Darwin |
| Canberra pia ni mji mkuu wa Australia | |

## Majimbo

**New South Wales** ilikuwa koloni ya kwanza kuanzishwa na Briteni. Sydney ni mji mkuu wa New South Wales na ndio mji mkubwa zaidi wa taifa. Harbour Bridge na Opera House ya Sydney ni ikoni za kitaifa.



New South Wales

**Victoria** ndio jimbo ndogo zaidi la nchi kuu. Majengo mengi mazuri huko Victoria yalijengwa kutoka kwa mali iliyoundwa na dhahabu ya 1850. Mji mkuu wa Victoria ni Melbourne.



Victoria

**Queensland** ni jimbo la pili kubwa. Ina visiwa vya Torres Strait kaskazini, misitu ya mvua, maeneo ya halijoto za pwani na nchi iliyokauka ya ndani. Mwamba Kuu wa Kuzuia unaojulikana zaidi ulimwenguni uko katika pwani ya mashariki. Mji mkuu wa Queensland ni Brisbane.



Queensland

**Australia Magharibi (Western Australia)** ndilo jimbo kubwa zaidi. Mashariki mwa jimbo ni jangwa sana, wakati kusini-magharibi ni eneo lenye ukulima na kukuza mvinyo. Jimbo hilo ni nyumbani kwa miradi mingi kubwa. Karibu robo tatu za idadi ya watu wa jimbo wanaishi huko Perth, mji mkuu.



Australia Magharibi

**Australia Kusini (South Australia)** ina pwani iliyochakaa na wilaya nyingi za mvinyo zinazojulikana. Adelide, mji mkuu, una mifano mingi ya usanifu majengo wa kikoloni.



Australia Kusini


**Tasmania** ndilo jimbo ndogo zaidi, imetengwa kutoka kwa nchi kuu na Bass Strait. Kisiwa kina mandhari ya jangwa ambayo hayajaharibiwa. Mji mkuu wa Tasmania ni Hobart.



Tasmania


## Wilaya

**Wilaya Kuu ya Australia (Australian Capital Territory)** iko katikati ya Sydney na Melbourne. Ni eneo la mji mkuu wa taifa, Canberra. Canberra ni nyumbani kwa taasisi muhimu za kitaifa, kama vile Jumba la Bunge na Mahakama Kuu ya Australia.



Wilaya Kuu ya Australia

**Wilaya ya Kaskazini (Northern Territory)** ina tropiki katika kaskazini na mchanga mwekundu wa jangwa huko kusini. Idadi nyingi ndogo inaishi katika mji mkuu, Darwin, karibu na barabara kuu kati ya Darwin na Alice Springs, ambayo ni jiji kuu karibu na Australia katikati.



Wilaya ya Kaskazini

# Tamaduni na ishara

## Siku muhimu kwa Australia

### Siku ya Australia

Mnamo 26 Januari kila mwaka, sisi husherehekea Siku ya Australia. Siku ya Australia ni sikukuu ya umma katika kila jimbo na wilaya hapa Australia.

Siku ya Australia, jamii kubwa na ndogo kote Australia husherehekea kila kitu nzuri kuhusu Australia na kuwa mtu wa Australia. Ndio tukio kubwa zaidi la kila mwaka hapa Australia.

Siku ya Australia ni siku ambayo huheshimu historia yetu na watu wote ambao wamefanya taifa hili kuwa kubwa. Ni siku ya kufurahia kwa mambo ya sasa na kujitolea kwa siku za usoni zenye furaha na ufanisi pamoja. Kwa sababu hii, ni siku ambayo hafla nyingi za uraia hufanywa kote nchini.

26 Januari ni siku ya makumbusho ya kuwasili kwa 'Kundi la kwanza la Meli (First Fleet) kutoka Briteni Kuu mnamo 1788 iliyowekwa kuanzisha makazi ya wafungwa kwa Serikali ya Briteni. Kamanda wa Kundi la kwanza la Meli (First Fleet) alikuwa Captain Arthur Phillip.

Usiku wa kuamkia Siku ya Australia, Waziri Mkuu hutangaza Tuzo ya Mwaustralia wa Mwaka huo huko Canberra.



Hafla nyingi za uraia hufanywa Siku ya Australia kila mwaka



Siku ya Gwaride la Anzac

### Siku ya Anzac

Siku ya Anzac hukumbukwa mnamo 25 Aprili kila mwaka. Siku ya Anzac imepewa jina baada ya Askari wa New Zealand na Australia, ambao walitua huko Gallipoli huko Uturuki wakati wa Vita vya I vya Dunia mnamo 25 Aprili 1915.

Siku ya Anzac ni siku ya zito wakati sisi hukumbuka thabihu ya Waaustralia wote ambao walitumikia na kufa siku za vita, shughuli za mizozo na utafutaji amani. Sisi pia huheshimu ujasiri na kujitolea kwa wanajeshi wote.

Maelezo zaidi kuhusu Siku ya Australia, Siku ya Anzac na siku zingine muhimu za kitaifa na sherehe zinaweza kupatikana katika *sehemu ya 4, Australia leo.*

# Bendera za Australia

Australia ina bendera tatu rasmi.: Bendera ya Kitaifa ya Australia, Bendera ya Watu wa Asili ya Australia na Bendera ya Watu wa Visiwa vya Torres Strait.

Kila jimbo na wilaya pia ina bendera. Hii inaweza kupatikana kwenye ukurasa wa 11.

## Bendera ya Taifa la Australia

Bendera ya Taifa ya Australia ni bluu, nyeupe na nyekundu. Ina sehemu tatu muhimu:

- Bendera ya Briteni Kuu, inayojulikana kama Union Jack, iko katika sehemu ya kona juu kushoto. Bendera inatoa mfano wa historia ya makazi ya Briteni.
- Nyota ya Jumuiya ya madola iko chini ya Union Jack. Nyota ina ncha saba, ncha moja kwa kila jimbo sita na moja ya wilaya.
- Msalaba wa Kusini (Southern Cross), sehemu ya kulia, ni kundi la nyota tunazoona angani.



Bendera ya Kitaifa ya Australia ni bluu, nyeupe na nyekundu

## Bendera ya Watu wa asili ya Australia

Bendera ya Watu wa asili ya Australia ni nyeusi, nyekundu na manjano. Ina sehemu tatu muhimu, na utafsiri unaojulikana zaidi wa rangi ni:

- Sehemu ya juu nusu ni nyeusi na inaiga watu wa asili wa Australia.
- Sehemu ya chini nusu ni nyekundu na inaiga ardhi na uhusiano wa kiroho wa nchi.
- Mviringo wa manjano inaiga jua.



Bendera ya Watu wa asili ya Australia ni nyeusi, nyekundu na manjano

## Bendera ya Watu wa visiwa wa Torres Strait

Bendera ya Watu wa visiwa wa Torres Strait ni kijani kibichi, bluu, nyeusi na nyeupe.

- Mistari ya kijani kibichi inaiga nchi.
- Paneli ya bluu iliyo katikati inaiga bahari.
- Mistari nyeusi inaiga watu wa visiwa vya Torres Strait.
- Kitambaa cheupe cha kichwa cha Mchezaji kilicho katikati ni ishara ya watu wote wa visiwa vya Torres Strait.
- Ncha za nyota nyeupe zinatoa mfano wa vikundi vya kisiwa katika Torres Strait.
- Rangi nyeupe ni ishara ya amani.



Bendera ya Watu wa visiwa wa Torres Strait ni kijani kibichi, bluu, nyeusi na nyeupe

## Nembo ya Jumuiya ya Madola

Nembo ya Jumuiya ya Madola ndio ishara rasmi ya Jumuiya ya Madola ya Australia. Inaleta mfano wa umoja wa kitaifa. Inatambua mamlaka na mali ya Jumuiya ya Madola ya Australia.

- Ngao katikati inaleta mfano wa majimbo sita na shirikisho.
- Kangaroo na emu inashikilia ngao kila upande. Kangaroo ni wanyama wenyeji wa Australia na emu ni ndege wenyeji wa Australia.
- Nyota ya dhahabu ya Jumuiya ya Madola hukaa juu ya ngao.
- Mandhari nyuma ni ufito wa dhahabu, maua ya kitaifa ya Australia.




Nembo ya Jumuiya ya Madola

## Maua ya kitaifa ya Australia


Maua ya kitaifa ya Australia ni ufito wa dhahabu. Mti huu mdogo hukua haswa katika kusini-mashariki Australia. Ina majani ya kijani kibichi na maua mengi ya manjano dhahabu wakati wa majira ya kuchipua. Kila jimbo na wilaya za Australia pia zina nembo yake ya maua.



Ufito wa dhahabu

## Rangi za kitaifa za Australia

Rangi za kitaifa za Australia ni kijani kibichi na dhahabu, rangi za ufito wa kijani kibichi. Sare za timu zetu za kitaifa za spoti kawaida ni kijani kibichi na dhahabu.



Rangi za kitaifa za Australia za kijani kibichi na dhahabu

## Kito cha kitaifa cha Australia

Opali ndio kito cha kitaifa cha Australia. Katika hadithi ya asili, upinde wa mvua uligusa ardhi na kuunda rangi za opali.



Opali

## Wimbo wa taifa wa Australia

'Endeleza Australia bila Mapendeleo' (Advance Australia Fair) ndio wimbo wa taifa. Huimbwa kwa hafla za umuhimu wa kitaifa. Pia huimbwa katika hafla za uraia wa Australia, matukio kuu ya michezo na shuleni. Inaunganisha taifa na ni onyesho la umma kwa raha na kujivunia kuwa Mwaustralia.

### Advance Australia Fair

*Australians all let us rejoice,*

*For we are young and free;*

*We've golden soil and wealth for toil;*

*Our home is girt by sea;*

*Our land abounds in nature's gifts*

*Of beauty rich and rare;*

*In history's page, let every stage*

*Advance Australia Fair.*

*In joyful strains then let us sing,*

*Advance Australia Fair.*

*Beneath our radiant Southern Cross*

*We'll toil with hearts and hands;*

*To make this Commonwealth of ours*

*Renowned of all the lands;*

*For those who've come across the seas*

*We've boundless plains to share;*

*With courage let us all combine*

*To Advance Australia Fair.*

*In joyful strains then let us sing,*

*Advance Australia Fair.*

* Ijapokuwa unaweza kujaribiwa kuhusu jina la wimbo wa kitaifa wa Australia, Hutajaribiwa kuhusu maneno ya wimbo wa kitaifa.






# Sehemu ya 2
# Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia

*Kuanzia wakati huu na kuendelea, chini ya Mwenyezi Mungu,**

*Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,*

***ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,***

***ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na***

*ambao nitafuata na kutii sheria zao.*

** Mtu anaweza kuchagua ikiwa atatumia maneno 'chini ya Mwenyezi Mungu'.*

# Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia

Kwenye hafla ya uraia, unaapa kwamba utashiriki imani za demokrasia za Australia na kwamba utaheshimu haki na uhuru wa watu wa Australia.

Australia ni demokrasia. Demokrasia ni mfumo wa serikali ambao raia huchagua kwa uhuru wawakilishi wa kuongoza nchi na kufanya sheria kwa niaba yao.

Australia wanaamini amani, heshima, uhuru na usawa. Sehemu muhimu ya kuwa Mwaustralia ni kuheshimu tofauti na chaguo za watu wengine, hata ikiwa haukubali na chaguo hizo. Ni juu ya kutendea watu bila mapendeleo na kuwapa Waaustralia fursa sawa na uhuru, haijalishi wanatoka wapi, tamaduni zao ni nini, au ikiwa ni waume au wake.

Imani za demokrasia hizi zimeunda nchi yetu na utamaduni wetu na ndio sababu watu wengi wanataka kuwa Waaustralia. Kwa hivyo ni muhimu kwamba uelewe imani hizi za demokrasia, na haki na uhuru ambao watu wote wa Australia wanazoheshimu.

# Imani zetu za demokrasia

## Demokrasia ya bunge

Mfumo wa serikali ya Australia ni demokrasia ya bungeni. Hii inaaanisha kwamba Waaustralia wote wanahusika katika jinsi nchi inaongozwa. Nguvu ya serikali inatoka kwa watu wa Australia kwa sababu raia wa Australia hupiga kura mara kwa mara kwa watu kuwawakilisha bungeni. Ni bunge tu ina nguvu ya kutengeneza na kubadilisha sheria ambazo zinaongoza nchi.

Katika demokrasia ya bungeni wawakilishi katika bunge lazima wajibu watu, kupitia Uchaguzi, kwa maamuzi wanayofanya.

## Utawala wa sheria

Sheria za Australia ni muhimu kwa watu wote wanaoishi Australia. Waaustralia wanatambua thamani ya sheria katika kukuza amani na jamii yenye mpangilio. Watu wote wa Australia wana haki ya kulindwa na sheria za Australia.

Kila mtu lazima atii sheria za Australia. Ikiwa hawatatii sheria, wanaweza kushikwa na polisi na lazima waende kortini.

Waaustralia wote ni sawa chini ya sheria na hakuna mtu au kundi liko juu ya sheria. Hii inaitwa 'utawala wa sheria'. Watu wenye vyeo vya juu katika jamii ya Australia lazima watii sheria za Australia. Hii ni pamoja na viongozi wa serikali, jamii na wa kidini, na watu wa biashara na polisi.

## Kuishi kwa amani

Tunajivunia kuishi katika nchi yenye amani na mfumo thabiti wa serikali. Tunaamini kwamba mabadiliko yanapaswa kutokea kupitia mjadala, ushawishi wenye amani na michakato ya demokrasia. Tunakataa uhasama kama njia ya kubadili mawazo ya mtu au sheria.

## Heshima kwa watu wote bila kujali asili

Watu huja kuishi Australia kutoka kwa nchi zote ulimwenguni. Watu wengi wana urithi tofauti wa kitamaduni na imani na mila tofauti. Katika jamii yetu ya kidemokrasia, tuko huru kufuata na kushiriki imani hizi na tamaduni bora tu zisizovunje sheria za Australia.

Tunathamini uhuru na tunatarajia Waaustralia wote kutendea wenzao na uadilifu na heshima, bila kujali kabila lao, nchi asili, jinsia, mapendeleo ya kingono, hali ya ndoa, umri, ulemavu, urithi, tamaduni, siasa, mali na dini.

Tunathamini heshima ya kawaida kwa uadilifu wa watu wote.

## Huruma kwa wale wanaohitaji

Hapa Australia, kuna roho ya 'kujali'. Hii inamaanisha tunasaidia na kupokea msaada kutoka kwa wengine nyakati za mahitaji. Mwenzako mara nyingi ni rafiki, lakini anaweza pia kuwa mtu usiojua kabisa. Mwenzako anaweza kula na jirani mzee, aendeshe rafiki kwenda kwa miadi ya matibabu au atembelee mtu aliye pweke.

Kwa sababu ya roho ya kujali, watu wengi na vikundi husaidiana kupitia kazi ya kujitolea ya jamii. Unaweza pia kuwa mtu wa kujitolea. Kazi ya kujitolea inaweza kutosheleza sana. Ni fursa kubwa pia kushiriki maarifa, kujifunza ustadi mpya, na kuongeza hali yako ya kuwa wa jamii ya Australia. Serikali yetu pia inasaidia Waaustralia wanaohitaji ruzuku ya serikali na huduma nyingine.

# Uhuru wetu

## Uhuru wa kuzungumza na uhuru wa kujielezea

Uhuru wa kuzungumza huruhusu watu kusema na kuandika wanachofikiria na kujadili mawazo yao na wengine. Uhuru wa kujielezea huruhusu watu kuonyesha maoni yao kupitia sanaa, sinema, muziki na fasihi.

Hapa Australia, tuko huru kusema na kuandika tunachofikiria, kwa usiri au hadharani, kuhusu mada yoyote. Walakini, hatuwezi kudhuru wengine.




Waaustralia wako huru kupinga maamuzi na sheria za serikali kwa amani

Hatuwezi kufanya malalamishi ya uwongo, hatuwezi kuhimiza wengine kuvunja sheria au kuharibu sifa za wengine. Kila wakati kuna sheria za kulinda jina zuri la mtu dhidi ya maelezo ya uwongo.

Ni kinyume na sheria kujaribu kufanya watu wengine wachukie au kutendea watu wengine uhasama kwa sababu ya utamaduni wao, kabila au asili.

Tuko huru kukutana na watu mahali pa umma au pa siri kwa mjadala wa kijamii au kisiasa. Tunaweza kukosoa serikali, kupinga kwa imani maamuzi ya serikali na kufanya kampeni kubadili sheria.

Lazima tusheshimu uhuru wa watu wengine wa kuzungumza au kujielezea.

Magazeti, runinga na redio zina uhuru sawa.

## Uhuru wa ushirika

Waaustralia wana uhuru wa kuungana na shirika la kisheria, kama vile chama cha kisiasa, chama cha wafanyikazi, kundi la kitamaduni au kijamii. Watu wanaweza pia kuamua kutojiunga nao.

Waaustralia wanaweza kuja pamoja kupinga hatua ya serikali au shirika. Walakini, malalamishi yote lazima yawe ndani ya sheria. Hii inamaanisha lazima ziwe za amani, na lazima zisiumize mtu yeyote au kuharibu mali.

## Uhuru wa dini na serikali ya kidunia

Australia ina urithi wa Ukristo wa Judea, na Waaustralia wengi hujielezea kama Wakristo. Australia ina sikukuu za umma kwa siku za Kikristo kama Ijumaa Kuu, Jumapili ya Pasaka na Siku ya Krismasi.

Walakini, serikali hapa Australia ni ya kidunia. Hii inamaanisha hakuna dini rasmi ya kitaifa.

Watu hapa Australia wako huru kufuata dini yoyote wanayochagua, bora desturi zake hazivunji sheria za Australia. Pamoja na Ukristo, Ubudha, Uislamu, Dini ya Kihindu, Uyahudi na dini zingine nyingi hufuatwa kwa uhuru Australia.

Australia ina uhuru wa kufuata dini. Serikali inatendea raia kwa usawa, haijalishi dini au imani yao.

Mchanganyiko wa dini nyingi huchangia kufanya Australia iwe ya nguvu na jamii yenye tamaduni anuwai.

Dini nyingi zina kanuni lakini hizo sio sheria za Australia. Kwa mfano, mchakato wa talaka, pamoja na ulinzi wa watoto na makazi ya mali, lazima yafuate sheria zilizopitishwa na Bunge la Australia. Watu wote wa Australia wana haki ya kulindwa na sheria hizi za Australia. Baadhi ya desturi za dini au tamaduni, kama vile kuolewa na zaidi ya mtu mmoja wakati mmoja, ziko kinyume na sheria ya Australia.

# Usawa wetu

## Usawa hapa Australia

Kuna baadhi ya sheria hapa Austrakia ambazo hukakikisha mtu hatendewi tofauti na wengine kwa sababu ya jinsia yao, rangi, ulemavu au umri.

## Usawa wa wanaume na wanawake

Wanaume na wanawake wana haki sawa hapa Australia. Ni kinyume cha sheria kubagua mtu kwa sababu ya jinsia yake.

Wanaume na wanawake wana haki ya kufanya uchaguzi wao binafsi kuhusu maswala kama ndoa, na wanalindwa na sheria ya dhuluma au uhasama.

Wanaume na wanawake wana ufikivu sawa wa elimu na ajira. Wanaume na wanawake wanaweza kupiga kura na kugombea bungeni. Wanaumena wanawake wanaweza jiunga na Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force) na polisi. Wanaume na wanawake wanatendewa sawa kortini na sheria.

## Usawa wa fursa

Waaustralia hawaamini vitengo vya utofauti katika jamii yetu. Badala yake, tunaamini jamii isiyopendelea, ambapo kila mtu anastahili "kutendewa sawa". Hii inamaanisha kwamba kile mtu anafikia maishani mwake kinapaswa kuwa matokeo ya bidii yao na vipawa vyao, kuliko mali na asili yao. Kwa mfano, mtu anapaswa kupata kazi au cheo kwa msingi wa ustadi wake, uwezo na uzoefu, sio kwa sababu ya asili yake.

Australia ina hadithi nyingi za wahamiaji wapya ambao wamekuwa viongozi katika biashara, wataalamu, sanaa, huduma ya umma na michezo kupitia bidii yao na vipawa vyao.



Watu huko Australia wako huru kufuata dini yoyote



Wanaume na wanawake wanaweza kuungana na Jeshi, Jeshi la Wanamaji na la Wanahewa



Waaustralia wote wana fursa ya kwenda kwa chuo kikuu

# Majukumu na fursa za uraia wa Australia

Kama mkaazi wa kukaa wa Australia, tayari umefurahia kuishi katika jamii huru ya kidemokrasia. Unapokuwa raia wa Australia, utakuwa na majukumu mapya. Pia utakuwa na fadhila anuwai mpya.

## Majukumu – utaipa Australia nini

Kama raia wa Australia lazima:

- utii sheria
- piga kura katika uchaguzi wa shirikisho na jimbo au wilaya, na katika kura ya maoni
- ulinde Australia ikiwa kutatokea hitaji
- utumikie katika baraza la wazee kortini unapoitwa kufanya hivyo.

## Fursa – Australia itakupa nini

Kama raia wa Australia, una haki ya:

- kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho na jimbo au wilaya, na katika kura ya maoni
- Kuomba kufanya kazi katika Huduma ya Umma wa Australia au katika Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force).
- kuwania uchaguzi wa bunge
- kuomba pasi ya Australia na kuingia tena Australia huru
- kupokea msaada kutoka kwa afisa wa Australia ukiwa ng'ambo
- kusajili watoto waliozaliwa ng'ambo kama raia wa Australia kwa ukoo.

# Majukumu

## Tii sheria

Wawakilishi wetu katika serikali hutengeneza sheria ili kukuza jamii yenye mpangilio, huru na salama na kulinda haki zetu. Waaustralia wote lazima watii sheria zinazoundwa na Bunge la Australia, bunge za jimbo na wilaya, na serikali za mtaa.

Maelezo zaidi kuhusu baadhi ya sheria muhimu hapa Australia zinaweza kupatikana katika *Sehemu ya 3, Serikali na sheria hapa Australia.*

## Piga kura katika uchaguzi wa shirikisho na jimbo au wilaya, na katika kura ya maoni

Upigaji kura ni haki muhimu kwa raia wote wa Australia. Tunapigia watu kura ambao tunataka watuwakilishe bungeni. Kwa kufanya hivi, tunaweza kusema jinsi nchi inaongozwa na kuchangia siku za usoni za Australia.

Kama raia, utapiga kura mara kwa mara katika uchaguzi wa jimbo na wilaya. Wakati mwingine, utapiga kura katika kura ya maoni, ambayo ni kura ya kubadili Katiba ya Australia. Maelezo zaidi kuhusu Katiba ya Australia zinaweza kupatikana katika *Sehemu ya 3, Serikali na sheria hapa Australia.*

Hapa Australia, upigaji kura ni lazima katika uchaguzi wa shirikisho na jimbo au wilaya. Raia wa Australia walio na miaka 18 au zaidi lazima wajaze fomu ya usajili wa uchaguzi kusajili jina lao na anwani kwenye orodha ya uchaguzi. Raia wa Australia wa miaka 18 na zaidi lazima wasajili majina na anwani zao kwenye orodha ya uchaguzi. Mara tu ukishakuwa kwenye orodha ya uchaguzi, kupiga kura ni lazima kwa raia wa Australia wenye miaka 18 na zaidi katika uchaguzi wa shirikisho na jimbo au wilaya.

Kupiga kura katika uchaguzi wa serikali sio lazima katika baadhi ya majimbo.




Tunaweza kusema kwa kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho, jimbo au wilaya na serikali ya mtaa

## Linda Australia ikiwa kutatokea hitaji

While service in the Australian Defence Force is voluntary, should the need arise it is vital that all Australian citizens be committed to joining together to defend the nation and its way of life.

### Tumikia baraza la wazee kortini ukiitwa kufanya hivyo

Huduma ya baraza la wazee inawajibika kwa raia wa Australia wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Baraza la wazee ni kundi la wanaume na wanawake wa kawaida wa Australia ambao husikiza ushahidi kortini na kuamua ikiwa mtu ana hatia au la.

Mwaustralia yeyote ambaye yuko kwenye jukumu la uchaguzi anaweza kuitwa kutumikia katika baraza la wazee.

Huduma ya baraza la wazee husaidia kuhakikisha kwamba mfumo wa korti ni wazi na usio na mapendeleo.

## Fursa

### Omba kazi katika Huduma ya Umma ya Australia na Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force)

Ikiwa wewe ni raia wa Australia, unaweza kuomba kujiunga na Huduma ya Umma na kufanya kazi kwa Serikali ya Australia kwa mfano, katika Centrelink, Medicare au ya Australian Taxation Office.

Raia wa Australia wana haki ya kuomba kwa taaluma katika Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force) (Jeshi, Jeshi la Wanamaji, na Wanahewa).

### Kuwania uchaguzi wa bunge

Raia wa Australia wa miaka 18 na zaidi wanaweza kuwania uchaguzi bungeni katika kiwango cha shirikisho, jimbo au wilaya. Ni heshima na jukumu kubwa kuhudumu katika bunge la Australia.

### Kuomba pasi ya Australia na kuingia tena Australia huru

Wakati umekuwa raia wa Australia, una haki ya kuishi huru Australia.

Una haki ya kuomba pasi ya Australia. Kama raia wa Australia, uko huru kusafiri ng'ambo na kurudi Australia. Hauhitaji visa kurudi Australia.

### Kupokea msaada kutoka kwa afisa wa Australia ukiwa ng'ambo

Katika nchi nyingi, Australia ina ubalozi, balozi kuu au kibalozi. Wakati uko ng'ambo, unaweza kuomba msaada kutoka kwa afisa wakati wa hitaji.

Hii ni pamoja na dharura kama mzozo wa kindani na maafa asilia. Maafisa wanaweza pia kutoa pasi za dharura na kutoa ushauri na msaada katika hali ya ajali, ugonjwa mkali au kifo.

Wakati uko katika nchi nyingine, lazima utii sheria za nchi hiyo.

### Sajili watoto waliozaliwa ng'ambo kama raia wa Australia kwa ukoo

Raia wa Australia wanaweza kuwa na watoto waliozaliwa ng'ambo. Wanaweza kusajili watoto wao kama raia wa Australia. Watoto basi wana haki sawa na majukumu ya uraia wa mtoto aliyezaliwa Australia.

## Kushiriki katika jamii ya Australia

Australia inahimiza raia wake wote kushiriki katika jamii. Raia ambao wanashiriki katika jamii wanachangia Australia kwa njia nyingi. Unaweza kujiunga na jamii za mtaa na eneo lako. Unaweza kujitolea kufanya kazi ya jamii na ustawi. Unaweza kujiunga shirika la sanaa au la utamaduni. Unaweza pia kushiriki kiamilifu katika maisha ya kisiasa.

Kulipa ushuru ni njia nyingine muhimu ya kuchangia moja kwa moja jamii ya Australia. Ushuru hulipwa kutoka kwa pesa unazopata, ikiwa ni kutoka kazini, biashara au vitega uchumi.

Fadhila nyingi ambazo Australia hufurahia leo huweseshwa kupitia ushuru. Ushuru hutumika kwa huduma ambazo ni pamoja na afya, elimu, ulinzi, barabara na reli, na ruzuku ya serikali. Kwa kufanya kazi na kulipa ushuru, unaweza kusaidia serikali kutoa huduma hizi muhimu kwa jamii ya Australia. Huduma hizi zinasaidia kufanya Australia kuwa nchi yenye amani na ufanisi leo. Serikali za jimbo na wilaya na baraza za mtaani pia hukusanya ushuru kupilia huduma.

Kulipa ushuru kunahitajika na sheria. Ushuru unakusanywa na Ofisi ya Ushuru ya Australia (ATO) kutoka biashara na watu binafsi. ATO hufanya kazi kuhakikisha raia wote wanajua haki zao za ushuru na majukumu yao kulipa kiwango sawa cha ushuru.





# Sehemu ya 3
# Serikali na sheria nchini Australia

*Kuanzia wakati huu na kuendelea, chini ya Mwenyezi Mungu,**

*Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,*

*ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,*

*ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na*

***ambao nitafuata na kutii sheria zao.***

** Mtu anaweza kuchagua ikiwa atatumia maneno 'chini ya Mwenyezi Mungu'.*

# Serikali na sheria nchini Australia

Katika hafla ya uraia, unaapa kufuata na kutii sheria za Australia. Ni muhimu kwako kuelewa mfumo wa serikali ya Australia, jinsi sheria huundwa katika bunge letu na jinsi sheria hizi hutekelezwa. Ni muhimu pia kuelewa jinsi, kama raia, utaweza kusema katika kuongoza nchi.

## Ninawezaje kusema?

### Upigaji kura

Hapa Australia, raia walio na miaka 18 na zaidi lazima wajiandikishe katika uchaguzi wa shirikisho. Kwa kupiga kura, unaweza kusema ni nani atakuwakilisha bungeni. Ikiwa haujajiandikisha sahihi, hauwezi kupiga kura katika uchaguzi.

Ukiwa katika orodha ya kupiga kura, upigaji kura ni lazima katika uchaguzi wa shirikisho la Australia na jimbo au wilaya. Usipopiga kura katika uchaguzi na hauna sababu nzuri ya kutopiga kura lazima ulipe faini. Upigaji kura kwa lazima ni njia ya kuhakikisha kwamba watu tunaochagua ni wao ambao watu wengi wanataka.

Australian Electoral Commission (AEC) ni chombo cha Jumuiya ya Madola. Huwa inafanya uchaguzi na kura za maoni na hukuza orodha ya uchaguzi wa Jumuiya ya madola. AEC husaidia kupea wapigaji kura uchaguzi usio na mapendeleo na wazi. AEC haitegemei serikali. Vyama vya kisiasa au watu katika serikali hawawezi kushawishi maamuzi ya AEC. Kura huwekwa katika sanduku za siri, kwa hivyo uko huru kupiga kura kwa mgombea wowote. Hakuna mtu mwingine anaona unapigia nani kura. Unaweza kuambia watu wengine unapigia nani kura, lakini hakuna mtu anaweza kukulazimisha kufanya hivyo.

### Kuibua maswala na wawakilishi wako

Hapa Australia, una haki ya kuibua maswala ambayo yanakuhusu na mwakilishi aliyeteuliwa. Maoni yako yanaweza basi kuzingatiwa na bunge wakati inafikiria sheria mpya au mabadiliko ya sheria zilizoko. Kwa mfano, ikiwa una maoni kuhusu jinsi ya kuboresha mfumo wa uhamaji, unaweza kufanya miadi ili kujadili na mbunge wa eneo lako. Unaweza pia kuandika barua inayoelezea maoni yako.

Katika njia hii, Waaustralia wa kawaida wanaweza kusema katika kuunda sheria na sera za serikali.

## Je! tuliundaje mfumo wetu wa serikali?

### Shirikisho

Kabla ya 1901, Australia ilikuwa na koloni sita tofauti za Briteni, zenye uongozi wa binafsi.

Katika mipaka yake, kila koloni ilikuwa na katiba lake na sheria zake kuhusu ulinzi, uhamaji, ada ya barua, biashara na usafiri.

Watu walitaka kuunganisha koloni kuunda taifa moja la Australia kwa sababu kadhaa. Biashara na usafiri kati ya koloni ulikuwa ghali na pole pole. Kutekeleza sheria kota kwa mpaka kulikuwa ngumu. Koloni tofauti pia zilikuwa na mfumo legevu wa ulinzi. Muhimu zaidi utambulisho wa kitaifa cha Australia kilikuwa kimeanza kuundwa. Timu za michezo zilikuwa zinawakilisha Australia kimataifa na utamaduni wa kipekee wa Australia ulianza katika nyimbo zinazojulikana, mashairi, hadithi na sanaa.

Kuunganisha taifa ilikuwa ngumu, lakini baada ya muda, wazo la Australia moja lilikwua ukweli. Waaustralia wanajivunia ukweli kwamba taifa lao halikutokea kupitia mapinduzi au umwagaji damu, lakini kwa kujadiliana na kura ya maoni.

Mnamo 1 Januari 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho la majimbo yanayoitwa Jumuiya ya Madola ya Australia.


## Katiba ya Australia

*Sheria ya Katiba ya Jumuiya ya Madola ya Australia 1990* ndio hati halali ambayo inaelezea sheria muhimu za serikali ya Australia. Katiba ya Australia ilipitishwa kama sehemu ya Sheria ya Bunge ya Briteni mnamo 1 Januari 1900. Mnamo 1 Januari 1901, wakati katiba ilianza, koloni za Australia zilikuwa taifa huru, Jumuiya ya Madola ya Australia.

Katiba ya Australia ilianzisha Bunge ya Jumuiya ya Madola ya Australia, iliyoundwa na Jumba ya Wawakilishi na Seneti. Katiba pia iliaanzisha Mahakama Kuu ya Australia, ambayo ina nguvu ya kutekeleza na kufafanua sheria za Australia.

Katiba ya Australia inaweza kubadilishwa kupitia kura maalum inayoitwa kura ya maoni.

Katika kura ya maoni, kunahitajika kuwa na idadi kubwa mara mbili ya watu kwa Katiba ya Australia kubadilishwa. Hii inamaanisha idadi kubwa ya wapigaji kura wa jimbo na idadi kubwa ya wapigaji kura kote nchini laizima wapige kura kwa badiliko hilo.




Katiba ya Australia

# Je! nguvu ya serikali inathibitiwa vipi?

Katiba ya Australia inagawanya nguvu kati ya mikono mitatu ya serikali. Hii ni kukomesha mtu mmoja au kundi moja la watu kuchukua nguvu ya kuongoza Australia.

### Nguvu ya kisheria

Bunge ina nguvu ya kutengeneza na kubadilisha sheria. Bunge ina wawakilishi ambao wamechaguliwa na watu wa Australia.

### Nguvu kuu

Nguvu kuu ni nguvu ya kutekeleza sheria. Wakuu ni pamoja na mawaziri wa Serikali ya Australia na Gavana Mkuu. Kila waziri ana jukumu la idara moja au zaidi za serikali.

### Nguvu za hakimu

Judges have the power to interpret and apply the law. Courts and judges are independent of parliament and government.

Nguvu zimeandikwa katika Katiba ya Australia.

# Je! ni nani ndiye Mkuu wa Nchi ya Australia?

Mkuu wa nchi ya Australia ni Malkia wa Australia, Mtukufu Malkia Elizabeth II.

Hapa Australia, Malkia sio lazima awe na jukumu la kila siku katika serikali. Malkia huteua Gavana Mkuu kama mwakilishi wake katika Australia, kwa ushauri kutoka kwa Waziri Mkuu wa Australia. Gavana Mkuu hutenda bila kutegemea vyama vyote vya kisiasa.

Katika kila jimbo kuna Gavana anayewakilisha Malkia katika jukumu ambalo ni sawa na Gavana Mkuu.

## Utawala wa Kikatiba

Australia is a constitutional monarchy. A constitutional monarchy is a country in which a king or queen is the head of state but has to act in accordance with the constitution.

Australia ni ufalme wa kikatiba. Ufalme wa kikatiba ni nchi ambapo mfalme au malkia ndiye mkuu wa nchi lakini lazima atende kulingana na katiba.

## Jukumu la Gavana Mkuu

Gavana Mkuu:

- usaini hati zote zinazopitishwa na Bunge la Australia kuwa sheria (hii inaitwa Idhini ya Kifalme)
- husaini kanuni
- huongoza kazi za hafla
- huidhinisha uteuzi wa Serikali ya Australia na mawaziri wake, majaji wa shirikisho na maafisa wengine.

Gavana Mkuu pia ana nguvu maalum zinazojulikana kama 'nguvu zilizotengwa' ambazo zinaweza tu kutumika katika hali mahususi.

# Je! ni nani baadhi ya viongozi wa Australia?

### Mkuu wa Nchi

Malkia wa Australia

### Gavana Mkuu

Mwakilishi wa Mkuu wa Nchi ya Australia

### Gavana

Mwakilishi wa Mkuu wa Nchi ya Australia katika kila jimbo

### Waziri Mkuu

Kiongozi wa Serikali ya Australia

### Mbunge Mkuu

Kiongozi wa serikali ya jimbo

### Waziri Mkubwa

Kiongozi wa serikali ya wilaya

### Waziri wa Serikali

Mbunge aliyeteuliwa na kiongozi wa serikali kuwajibikia eneo la serikali.

### Mbunge (MP)

Mwakilishi aliyeteuliwa na watu wa Australia katika bunge la Australia.

### Seneta

Mwakilishi aliyeteuliwa wa jimbo au wilaya katika Bunge la Australia.

### Meya au Rais wa Mkoa

Kiongozi wa baraza la mtaa

### Diwani

Mwanachama aliyeteuliwa na baraza la mtaani



Nyumba mzee ya Bunge huko Canberra ilifunguliwa mnamo 1927

# Je! Australia inaongozwa vipi?

## Serikali ya Australia

Serikali ya Australia pia inaitwa Serikali ya Shirikisho au Serikali ya Jumuiya ya Madola.

Bunge la Australia lina Nyumba mbili:

- Jumba la Wawakilishi
- Seneti.

Wanachama wa nyumba zote mbili huteuliwa moja kwa moja na watu wa Australia katika uchaguzi wa shirikisho. Wakati unapiga kura katika uchaguzi wa shirikisho, kawaida wewe huteua wawakilishi wa kila Jumba.



Nyumba mpya ya Bunge huko Canberra ilifunguliwa mnamo 1988

## Wawakilishi wa Jumba

Wawakilishi wa Jumba nyakati zingine hujulikana kama Jumba la Chini au Jumba la Watu.

Australia imegawanywa katika makundi ya shirikisho ya wapigakura. Waaustralia katika kila kundi la wapigakura hupigia kura mtu mmoja kuwa kuwawakilisha katika Jumba la Wawakilishi. Mwakilishi huyu huitwa Mbunge (MP).

Idadi ya Wabunge kwa kila jimbo na wilaya huwa kwenye msingi wa saizi ya idadi. Watu wa Australia huchagua jumla ya wanachama 150 kwa Jumba la Wawakilishi.

Kazi muhimu ya Jumba la Wawakilishi ni kuzingatia, kujadili na kupiga kura mapendekezo ya sheria mpya au mabadiliko ya sheria. Wanachama wa Jumba wa Wakilishi pia hujadili maswala ya umuhimu wa taifa.



Wawakilishi wa Jumba

## Seneti

Seneti nyakati zingine huitwa Jumba la Juu, Jumba la Kuhakiki au Jumba la Majimbo.

Majimbo huwakilishwa katika Seneti, haijalishi saizi ya idadi ya watu. Kuna wawakilishi 12 walioteuliwa kutoka kila jimbo. Wilaya zote mbili huteua wakilishi wawili. Kuna wakilishi 76 walioteuliwa na wanaitwa Maseneta.

Maseneta pia huzingatia, hujadili na kupigia kura sheria mpya au mabadiliko ya sheria. Maseneta pia hujadili maswala ya umuhimu wa taifa.



Seneti

## Serikali ya jimbo na wilaya

Kuna majimbo sita na wilaya mbili za nchi kuu hapa Australia. Kila jimbo lina katiba yake na bunge lake. Serikali za jimbo na wilaya ziko kwa msingi wa miji yao mikuu.

Kiongozi wa serikali ya kimbo ni Mbunge mkuu na kiongozi wa serikali ya wilaya ni Waziri Mkubwa.

Serikali za Jimbo huendeshwa kwa njia sawa na Serikali ya Australia. Katika kila jimbo, Gavana huwakilisha Malkia wa Australia. Katika Wilaya ya Kaskazini, Msimamizi huteuliwa na Gavana Mkuu. Wajibu na majukumu ya Msimamizi ni sawa na zile za Gavana wa jimbo.

Kama Serikali ya Australia, watu hupiga kura kuchagua mwakilishi wa eneo lao. Wawakilishi huwa mwanachama wa bunge ya jimbo au wilaya.

## Serikali za mitaa

Majimbo na Wilaya za Kaskazini zimegawanywa katika maeneo ya serikali ya mitaa. Hizi zinaweza kuitwa miji, mikoa au manispaa. Kila eneo lina baraza lake la mtaa. Baraza zinawajibika kwa kupanga na kuwasilisha huduma kwa jamii yake ya eneo. Raia katika kila eneo la serikali za mitaa hupiga kura kuteua madiwani wao wa mitaa.

# Je! viwango tatu vya serikali hufanya nini?

Serikali ya Australia inawajibika kwa:

- ushuru
- usimamizi wa uchumi wa kitaifa
- uhamaji na uraia
- ajira
- huduma za posta na mtandao wa mawasiliano
- ruzuku ya serikali (pensheni na msaada wa familia)
- ulinzi
- biashara
- uwanja wa ndege na usalama wa angani
- maswala ya nje (mahusiano na nchi zingine).



Serikali ya Australia inawajibika kwa usimamizi wa uchumi wa kitaifa

Serikali za jimbo na wilaya zinawajibika kwa:

- hospitali na huduma za afya
- shule
- reli
- barabara na uthibiti wa trafiki ya barabara
- misitu
- polisi
- uchukuzi wa umma.



Serikali za jimbo na wilaya zinawajibika kwa hospitali

Serikali za (na Serikali ya Mpaka Mkuu wa Australia) mitaa zinawajibika kwa:

- Ishara za mitaa, vithibiti trafiki
- barabara za mitaa, njia, daraja
- mifereji
- mbuga, viwanja vya michezo, madimbwi ya kuogelea, viwanja
- viwanja vya kupiga kambi na misafara
- uchunguzi wa chakula na nyama
- uhibiti wa kelele na wanyama
- ukusanyaji taka
- maktaba, ukumbi na vituo vya jamii wa mitaa
- maswala fulani ya utunzaji wa watoto na wazee
- hati za kujenga
- mipango ya jamii
- maswala ya mazingira ya mitaa.



Serikali za mitaa zinawajibika kwa viwanja vya michezo

Majukumu mengine hushirikishwa kati ya viwango anuwai za serikali. Council of Australian Government (COAG) imewekwa kuhimiza ushirikiano kati ya viwango vya serikali.

## Je! vyama vya kisiasa vina jukumu gani katika njia Australia inavyoongozwa?

Chama cha kisiasa ni kundi la watu wanaoshiriki maoni sawa juu ya vile nchi inapaswa kuongozwa. Wao hufanya kazi pamoja kubadili maoni ya chama kuwa sheria. Vyama kuu vya kisiasa hapa Australia ni Chama cha Wafanyikazi cha Australia (Australian Labor Party), Chama cha Uhuru cha Australia (Liberal Party of Australia), Wakitaifa (Nationals) na Kijani kibichi cha Australia (Australian Greens).

Wabunge wengi wako katika vyama vya kisiasa. Baadhi ya wabunge hawako katika chama chochote cha kisiasa. Wanajulikana kama Wanaojitegemea.

Hapa Australia, uko huru kujiunga na chama chochote cha kisiasa ukichagua.

## Je! Serikali ya Australia inaundwa vipi?

Baada ya uchaguzi, chama cha kisiasa au muungano wa vyama ulio na wanachama wengi kwenye Jumba la Wawakilishi huunda Serikali ya Australia. Kiongozi wa chama hiki huwa kiongozi wa Serikali ya Australia, Waziri Mkuu.

Chama au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kubwa ya wanachama kwenye Jumba la Wawakilishi inajulikana kama Wapinzani. Kiongozi wake anajulikana kama Kiongozi wa Upinzani.

Waziri mkuu huchagua Wabunge au Seneta kuwa mawaziri. Mawaziri huwajibika kwa maeneo muhimu ya serikali (inajulijkana kama orodha ya kazi) kama ajira, maswala ya Watu wa asili, au Hazina. Mawaziri walio na Uwaziri mkubwa zaidi huunda Baraza la mawaziri, ambalo ndio funguo la halmashauri ya uamuzi wa Serikali ya Australia.



Mahakama Kuu ya Australia

## Je! sheria huundwa vipi?

Raia wa Australia huchagua watu kuwawakilisha katika Bunge la Australia.

Bunge la Australia huunda na kubadilisha sheria kufaidisha taifa.

Mbunge wa Bunge la Australia hupendekeza sheria mpya au mabadiliko kwa sheria. Pendekezo hili huitwa Mswada.

Jumba la Wawakilishi na Seneti huzingatia, hujadili na hupiga kura ikiwa wanakubali Mswada.

Ikiwa idadi kubwa ya watu katika Jumba la Bunge wanakubali Mswada, huwa inaenda kwa Gavana Mkuu.

Wakati Gavana Mkuu anatia saini Mswada, huwa inakuwa sheria. Hii inaitwa Idhini ya Kifalme.

Bunge za Jimbo na wilaya huunda sheria zao kwa njia sawa.

## Je! sheria hutekelezwa vipi?

### Korti

Korti za Australia zinawajibika kwa kufafanua na kutekeleza sheria. Hazitegemei serikali. Korti huamua ikiwa mtu amevunja sheria au sivyo na huamua adhabu. Kila mtu ana haki ya kuwakilishwa na wakili kortini. Korti zinaweza kuweka maamuzi yao kwa msingi wa ushahidi ulio mbele yao.

### Majaji na mahakimu

Jaji au hakimu mkuu ndiye mamlaka ya juu kortini. Majaji ya mahakimu wanajitegemea na hakuna mtu anaweza kuwaambia cha kuamua.

Majaji na mahakimu huteuliwa na serikali, lakini serikali haiwezi kuchukua kazi zao ikiwa haikubaliani na maamuzi yao.

## Baraza la wazee la Mahakama

Korti itatumia baraza la wazee katika hali zingine kuamua ikiwa mtu amevunja sheria.

Baraza la wazee ni kundi la watu wa kawaida ambao huchaguliwa bila uratibu kutoka kwa idadi ya watu. Jaji hufafanua sheria kwa baraza la wazee. Katika usikilizaji wa uhalifu, baraza la wazee wakipata mtu ana hatia, jaji huamua adhabu.

Chini ya sheria, watu wa Australia wanazingatiwa kutokuwa na hatia hadi wapatikane wana hatia na korti.

## Polisi

Polisi hukuza amani na mpangilio katika jamii. Ni kazi yao kulinda maisha na mali. Hawategemei serikali. Ikiwa polisi wanaamini kwamba mtu amevunja sheria, wanaweza kuwashika na kuwaleta mbele ya korti ya sheria. Polisi wanaweza kupeana ushahidi kortini, lakini korti huamua ikiwa mtu ana hatia au la.

Majimbo na Wilaya za Kasazini zina jeshi lao la polisi. Wao hushugulika na uhalifu chini ya sheria za jimbo na wilaya.

Australia pia ina polisi la kitaifa linaloitwa Polisi wa Shirikisho wa Australia. Polisi wa Shirikisho wa Australia huchunguza uhalifu dhidi ya sheria la shirikisho, kwa mfano, ulanguzi wa madawa ya kulevya, uhalifi dhidi ya usalama wa taifa na uhalifu dhidi ya mazingira. Polisi wa Shirikisho wa Australia pia wanawajibikia kazi ya jumla ya polisi katika Wilaya Kuu ya Australia.

Polisi na jamii wana uhusiano mwema nchini Australia. Unaweza kuripoti uhalifu na kutafuta msaada kutoka kwa polisi wa eneo lako.

Ni muhimu kwako kuzoea sheria za Australia, kwa sababu kutojua sheria sio sababu ya kuivunja.

Ni hatia kubwa kuhonga afisa wa polisi. Ni hatia hata kupeana hongo kwa afisa wa polisi.

## Hatia za uhalifu hapa Australia

Baadhi ya hatia mbaya zaidi ni pamoja na kuua, kuvamia, kuvamia cha kingono, uhasama dhidi ya watu au mali, wizi wa mabavu au wizi, kuwa na uhusiano wa kingono na watoto au vijana ambao wako chini ya umri halali, uendeshaji hatari wa gari, umiliki na utumizi wa madawa ya kulevya na utapeli.

Kama vile katika nchi zingine, uhasama kwa mtu mwingine ni kinyume cha sheria nchini Australia na ni uhalifu mbaya sana. Hii ni pamoja na uhasama nyumbani na katika ndoa, inayojulikana kama uhasama wa jamii. Uhasama wa nyumbani ni pamoja na dhuluma au kudhurika ya kimwili, kingono au kisaikolojia, uhusiano uliolazimishwa wa kingono, kutengwa kuliolazimishwa au kunyimwa kiuchumi.

Kubeba silaha kama vile visu au bunduki ni kinyume na sheria hapa Australia. Mtu anayetaka kumiliki bunduki kwa mfano, kwa utumizi kwa shamba, lazima apate leseni ya silaha kutoka kwa polisi.

## Hatia za Trafiki

Sheria za trafiki na barabara huthibitiwa na serikali za jimbo na wilaya. Watu wanaweza kuitishwa faini kubwa za pesa au hata kutumwa jela kwa kuvunja sheria za trafiki. Kuendesha gari Australia, lazima uwe na leseni ya kawaida ya kuendesha gari na lazima gari limesajiliwa.

Kila mtu anayesafiri kwa gari lazima avae mkanda. Watoto wachanga lazima wawekwe katika kiti cha gari kilichoidhinishwa. Sheria za tarfiki zinazohusiana na kuendesha na mwendo mkali na baada ya kunywa pombe au madawa ya kulevya ni kali mno. Ni kinyume na sheria pia kuzungumza na simu ya mkononi unapoendesha gari.

# Kwa kutamatisha

Taasisi zetu za kidemokrasia zimeunda jamii yenye amani na thabiti. Tuna utamaduni mzuri na wa kipekee kushiriki. Kama raia wa Australia, utakuwa sehemu ya hadithi yetu ya kitaifa na utachangia siku za usoni. Australia inakukaribisha. Uraia ni mapatano yetu ya pamoja.

Katika kujiandaa kwa jaribio la uraia, jaribu kujifunza maswali ya jaribio kwenye ukurasa wa 34 na 35.

# Faharasa ya maswali yanayoweza kujaribiwa

**Huduma ya Umma ya Australia**
idara za serikali na watu walioajiriwa nazo
*Paul alipata kazi katika Huduma ya Umma ya Australia kama afisa wa Centrelink.*

**mzozo wa umma**
maandamano na vurugu na idadi kubwa ya watu, kawaida kupinga dhidi ya uamuzi au sera ya serikali
*Kulikuwa na mzozo wa umma wakati serikali ilipitisha sheria zisizojulikana.*

**muungano**
kuungana na vyama viwili au zaidi, kawaida kuunda serikali au upinzani
*Baada ya uchaguzi, hakuna chama kilicho na watu wengi katika Jumba la Wawakilishi, kwa hivyo vyama viwili vya maoni sawa viliunganisha kuunda muungano.*

**tume**
kundi la watu walio na jukumu rasmi
*Tume inayojitegemea huandaa uchaguzi.*

**ufalme wa kikatiba**
nchi ambapo mfalme au malkia ndiye mkuu wa nchi, ambaye nguvu zake zimezuiliwa na katiba
*Katiba yetu ilianzisha Jumuiya ya Madola ya Australia kama utawala wa kikatiba, na Mfalme au Malkia wa Uingereza kama Mkuu wa Serikali yetu.*

**korti**
mahali ambapo kesi za kisheria huongozwa na jaji au hakimu
*Wakati watu wanavunja sheria, wanaweza kwenda kortini.*

**usiklizaji wa uhalifu**
usikilizaji wa ukweli wa korti juu ya uhalifu uliodaiwa ikiwa mtu amepatikana na hatia au hana hatia
*Baada ya usikilizaji wa hatia, mwizi wa benki alitumwa kwa jela.*

**demokrasia**
serikali na watu kupitia wawakilishi walioteuliwa
*Grace alifurahia kuishi katika demokrasia ambapo angeweza kupigia kura kwa mwakilishi wake bungeni.*

**ulanguzi wa madawa ya kulevya**
kubeba au kununua madawa ya kulevya kinyume ya sheria
*Jess alitumwa jela kwa ulanguzi wa madawa ya kulevya.*

**kunyimwa kiuchumi**
aina ya uhasama wa nyumbani, ambapo mtu mmoja katika uhusiano anazuia mwingine kupokea au kushughulikia pesa
*Lin alipitia kunyimwa kiuchumi kwa saabu mume wake hakumpa pesa zozote.*

**uchaguzi**
tukio ambalo raia huchagua mtu wa kuwawakilisha katika bunge
*Raia wa Australia wenye umri wa miaka 18 na zaidi lazima wapige kura katika uchaguzi.*

orodha ya uchaguzi
orodha ya watu wanaoweza kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni
*Wakati Jan alifika katika kituo cha kupigia kura, afisa alitafuta jina lake kwenye orodha ya uchaguzi.*

tekeleza sheria
kuhakikisha kwamba watu wanafuata sheria
*Polisi hutekeleza sheria na kuhimiza amani.*

nguvu kuu
nguvu na mamlaka ya kutekeleza sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Mawaziri wa Serikali ya Australia na Gavana Mkuu wana nguvu kuu ya kutekeleza sheria zilizoundwa na Bunge la Australia.*

shirikisho
muungano wa koloni katika taifa moja iliyo na koloni zilizozuia nguvu fulani
*Mnamo 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho liitwalo Jumuiya ya Madola ya Australia.*

Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet)
kundi la meli 11 zilizotoka kwenda Briteni chini ya Captain Arthur Phillip kuanzisha makazi ya wafungwa huko New South Wales
*Siku ya Australia sisi hukumbuka kutua kwa Kundi la kwanza la Meli (First Fleet) huko Sydney Cove mnamo Januari 26 1788.*

Ishara ya maua
maua ya kitaifa
*Ishara ya maua ya Australia ni ufito wa dhahabu.*

kutengwa kwa kuliolazimishwa
aina ya uhasama wa nyumbani ambapo mtu mmoja wa uhusiano anathibiti nani mwenzake anaona na kuzungumzia, nini anasoma na mahali anaenda
*Sandi alilazimishwa kutengwa kwa sababu mume wake haukumruhusu kutembelea marafiki au familia.*

kuanzia sasa na kuendelea
kuanzia sasa na siku za usoni
*Katika hafla ya uraia, unaahidi kuwa mwaminifu wa Australia kuanzia sasa na kuendelea.*

ikoni
picha inayojulikana
*Jumba la Opera ni ikoni inayojulikana ya Sydney.*

Watu wa asili
wakazi asili wa nchi – huko Australia, watu wa asili na wakazi wa visiwa vya Torres Strait
*Watu wa asili ya Australia huunda asilimia 2.5 ya idadi ya watu wa Australia.*

Yahudi-Kikristo
wenye dini za Wayahudi na Wakristo
*Thamani za Yahuhi-Kikristo ni zenye msingi wa kutoka kwa Biblia.*

nguvu za kisheria
nguvu na mamlaka ya kufafanua na kutekeleza sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Korti huko Australia zina nguvu ya kisheria kufafanua na kutekeleza sheria.*

lnguvu ya kutunga sheria
nguvu na mamlaka ya kuunda na kubadili sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Chini ya katiba, bunge ina nguvu ya kutunga sheria, hiyo ni nguvu ya kuunda sheria.*

uhuru
uhuru wa kibinafsi na uhuru
*Katika jamii yetu ya demokrasia, watu wana uhuru wa kuzungumza, uhuru wa kujielezea, uhuru wa dini na uhuru wa ushirika. Tunathamini uhuru huo.*

hakimu mkuu
jaji (kiongozi) wa korti ya kiwango cha chini
*Hakimu mkuu alipata mwizi na hatia na kumtuma kwa jela.*

kujali
kusaidia na kupokea msaada kutoka kwa wengine, haswa katika nyakati ngumu
*Wakati gari langu liliharibika, madereva wengine walitusaidia kulisukuma katika moyo wa kujali.*

wimbo wa taifa
wimbo wa taifa
*Wimbo wa taifa wa Australia ni 'Eendeleza Australia bila Mapendeleo' (Advance Australia Fair).*

demokrasia ya bunge
mfumo wa serikali ulio kwenye msingi wa uchaguzi wa kawaida wa wawakilishi wa bunge na raia
*Katika demokrasia ya bunge, watu hupiga kura kwa wawakilishi wao.*

raia wa kudumu
mtu ambaye ana visa ya kuishi na kufanya kazi nchini Australia bila kizuizi chochote muda
*Jirani Mjapani wa Abdul ni raia wa kudumu wa Australia na anafanya kazi kwa benki.*

chama cha kisiasa
ni kundi la watu wanaoshiriki maoni sawa juu ya vile nchi inapaswa kuongozwa
*Wanachama wa chama cha kisiasa hukutana mara kwa mara, kwa mfano, kujadili kuboresha uchukuzi wa umma.*

huduma ya umma
utumizi wa wakati, nguvu au ustadi kwa uzuri wa taifa
*Jose alitoa huduma ya umma kwa kusaidia wakimbizi kukaa Australia.*

kura ya maoni
kura na wapigaji kura wote kwenye mabadiliko yaliyopendekezwa katika Katiba ya Australia
*Katika kura ya maoni 1967, watu walipiga kura kuhesabu watu wa asili ya Australia kwenye sensa.*

mwakilishi
mtu ambaye hutenda au kusema kwa niaba ya wengine
*Mwakilishi wa baraza la eneo langu alipenda maoni yangu na aliwakilisha katika mkutano wa baraza.*

kuhakiki
kuzingatia pendekezo kwa sheria mpya na kuamua ikiwa kuikubali au kuikataa
*Seneti, kama Jumba la Kuhakiki, kujadili Mswada wa ushuru kutoka kwa Jumba la Chini.*

sanduku la siri
mfumo wa kupiga kura ambapo watu hupiga kura kwa siri, ili hakuna mtu anaweza kushawishi au kushinikiza mwingine kupiga kura kwa njia fulani
*Katika sanduku la siri hakuna mtu anayetazama unapoandika kura yako.*

kidunia
kando na dini
*Katika jamii ya kidunia hakuna dini rasmi.*

mpangilio
kujenga, kukuza, kuanza
*Gavana Philip alianza koloni ya kwanza huko New South Wales.*

mkoa
eneo la serikali ya mitaa
*Barabara katika mkoa wangu ni salama sana.*

ruzuku ya serikali
malipo ya pensheni au fadila za serikali kusaidia watu ambao hawana kazi, walemavu, wazee na wengine wanaohitaji
*Wakati Trang alipoteza kazi yake alikuwa ameomba ruzuku ya serikali.*

jaribu bahati yako
kujaribu
*Kila mwaka, mimi hujaribu bahati yangu mimi hufanya dau $10 kwenye farasi katika Kombe la Melbourne.*

mtu wa kujitolea
mtu anayepeana muda wake kwa mtu au shirika bila kutarajia malipo
*Raza ni mtu wa kujitolea anayefunza watu Kiingereza nyumbani kwao.*

# Maswali ya kweli yanayoweza kujaribiwa



## Australia na watu wake

### 1. Sisi hukumbuka nini Siku ya Anzac?

a. Kutua kwa Askari wa Jeshi wa Australia na New Zealand huko Gallipoli, Uturuki

b. Kuwasili kwa wakazi huru wa kwanza kutoka Briteni Kuu

c. Kutua kwa Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet) hapa Sydney Cove

### 2. Ni rangi zipi za Bendera ya Watu wa asili wa Australia?

a. Nyeusi, nyekundu na manjano

b. Kijani kibichi, nyeupe na nyeusi

c. Bluu, nyeupe na kijani kibichi

### 3. Ni ishara ipi rasmi ya Australia hutambua mali ya Jumuiya ya madola?

a. Wimbo wa taifa

b. Maua ya kitaifa ya Australia

c. Nembo ya Jumuiya ya Madola



## Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia

### 4. Ni ipi kati ya taarifa hizi juu ya mfumo wa serikali ya Australia ni sahihi?

a. Malkia wa Australia huchagua watu kuunda Bunge la Australia

b. Serikali huchaguliwa na watu

c. Waziri Mkuu huchagua Wabunge wetu

### 5. Ni ipi kati ya hizi ni mfano wa uhuru wa kuzungumza?

a. Watu wanaweza kufanya maandamano ya amani dhidi ya maamuzi ya serikali

b. Wanaume na wanawake hutendewa sawa kortini

c. Waaustralia wana uhuru wa kutofuata dini.

### 6. Ni ipi kati ya taarifa hizi juu ya serikali ya Australia ni sahihi?

a. Serikali hairuhusu dini zingine

b. Serikali nchini Australia ni ya kidunia

c. Sheria za kidini hupitishwa na bunge

### 7. Ni ipi kati ya hizi ni mfano wa usawa Australia?

a. Kila mtu hufuata dini sawa

b. Wanaume na wanawake wana haki sawa

c. Kila mtu ni wa chama sawa cha kisiasa

### 8. Ni ipi kati ya hizi ni jukumu la raia wa Australia wa umri wa miaka 18 au zaidi?

a. Kuhudhuria mikutano ya baraza la mitaa

b. Kupiga kura katika uchaguzi

c. Kuwa na pasi ya sasa ya Australia

### 9. Ni ipi kati ya hizi ni jukumu la raia wa Australia wa umri wa miaka 18 au zaidi?

a. Kufanya huduma za jamii ya eneo

b. Kubeba pasi wakati wote

c. Kutumikiwa katika baraza la wazee kortini anapoitwa kufanya hivyo

### 10. Ni ipi kati ya taarifa hizi juu ya pasi ni sahihi?

a. Raia wa Australia wanaweza kuomba pasi ya Australia

b. Wakazi wa kudumu wanaweza kuwa na pasi ya Australia

c. Raia wa Australia wanahitaji pasi na visa kurudi Australia



## Serikali na sheria Australia

### 11. Ni ipi kati ya taarifa hizi juu ya kupiga kura katika uchaguzi wa Australia ni sahihi?

a. Watu wako huru na salama kupiga kura kwa mgombea yeyote

b. Kupiga kura kwa kuinua mikono

c. Lazima watu waandike majina yao kwa kura yao

### 12. Ni nini kilitendeka huko Australia mnamo 1 Januari 1901?

a. Katiba ya Australia ikibadilishwa na kura ya maoni

b. Katiba ya Australia ilianza kufanya kazi

c. Askari wa Jeshi la Australia na New Zealand ilianzishwa

### 13. Jina la hati halali ambayo hutoa sheria kwa serikali ya Australia ni nini?

a. Shirikisho la Australia

b. Jumuiya ya madola ya Australia

c. Katiba ya Australia

### 14. Je! kura ya maoni ni nini?

a. Kura ya kubadili serikali

b. Kura ya kubadili Katiba ya Australia

c. Kura ya kubadili Waziri mkuu

### 15. Ni mkono upi wa serikali una nguvu ya kufafanua na kutekeleza sheria?

a. Watunga sheria

b. Wakuu

c. Mahakama

### 16. Ni ipi kati ya hizi ni jukumu la Gavana Mkuu?

a. Uteuzi wa wakuu wa jimbo

b. Kutia saini Miswada iliyopitishwa na Bunge la Australia

c. Uteuzi wa Mkuu wa Nchi

### 17. Ni ipi kati ya taarifa hizi juu ya serikali ya jimbo ni sahihi?

a. Majimbo yote yana katiba sawa

b. Kila jimbo lina katiba yake

c. Majimbo hayana katiba

### 18. Ni jina lipi hupewa chama au muungano wa vyama ambavyo vina idadi kubwa zaidi ya pili ya wawakilishi wa bunge?

a. Serikali

b. Upinzani

c. Seneti

### 19. Ni jina lipi la pendekezo kuunda sheria bungeni?

a. Idhini ya Kifalme

b. Mswada

c. Mjadala

### 20. Nani hukuza amani na mpangilio hapa Australia?

a. Wafanyikazi wa umma

b. Polisi

c. Wanasheria

Majibu:
1a, 2a, 3c, 4b, 5a, 6b, 7b, 8b, 9c, 10a, 11a, 12b, 13c, 14b, 15c, 16b, 17b, 18b, 19b, 20b

# Mwisho wa maswali yanayoweza kujaribiwa